

## Taarifa ya Ukuaji wa Mgodini ndani ya Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Tano

Sekta ya madini ni miongoni mwa sekta zilizokuwa kwa kasi ndani ya uongozi wa serikali ya awamu ya tano chini ya uongozi wa Rais Dkt. John Joseph Pombe Magufuli na kupelekea hata mchango wa kampuni ya kipekee ya Stamigold kuonekana na kuthaminika.



Kwa wasioifahamu vizuri, STAMIGOLD Company Limited ni kampuni tanzu ya Shirika la Madini la Taifa (STAMICO). STAMIGOLD ilianzishwa tarehe 28 mwezi Oktoba, 2013 kwa lengo la kusimamia shughuli za uendeshaji wa mgodi wa dhahabu wa Biharamulo (STAMIGOLD Biharamulo Mine “SBM”). Ni mgodi wa kipekee wa dhahabu nchini unaoendeshwa na kusimamiwa kwa asilimia

mia moja na watanzania.

Serikali kupitia STAMICO iliingia makubaliano ya kuchukua mgodi wakati ukijulikana kwa jina la Tulawaka Gold Mine kutoka kwa Kampuni ya Pangea Minerals Limited. Uzalishaji wa dhahabu mgodini chini ya usimamizi wa kampuni ya STAMIGOLD ulianza mwezi Julai, 2014.

STAMIGOLD imeendelea na shughuli za uzalishaji ambao ulianza kuyumba kipindi cha miaka ya 2015-2017, na inamshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuipigania ili mgodi huo uweze kuendelea kuzalisha dhahabu kulingana na mashapo yaliyohakikiwa na kwa utafiti uliokuwa bado unaendelea. STAMIGOLD Biharamulo Mine ina kila sababu ya kuishukuru serikali ya awamu ya tatu kwa kuisaidia kutatua changamoto mbali mbali kama kupunguza



gharama za nishati kwa kuanzisha mradi wa kunganisha mgodi kwenye Mkongo wa Umeme wa Taifa.



Shughuli zote za kufikisha miundo mbinu zimeshaanza na zinatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2020 ambapo Mradi mzima unatarajiwa kukamilika Mwezi Desemba mwaka huu kwa gharama ya shilingi za kitanzania bilioni 9.6 kutoka serikalini. Katika kuendeleza shughuli zake; Mgodini unatumia shilingi za kitanzania bilioni 1.01 kila mwezi kununulia mafuta ya *diesel* ili kuendesha shughuli mbalimbali lakini endapo mradi huo utakamilika basi mgodini utatumia shilingi milioni 300 kila mwezi na hivyo kuokoa takribani shilingi milioni 700 kila mwezi. Bodi ya wakurugenzi ya

TANESCO ilifanikiwa kufika mgodini mwezi Februari mwaka huu na kujionea shughuli mbali mbali na kuwahidi wafanyakazi uunganishaji wa mgodi kwenye mkongo wa umeme wa taifa na hivyo tatizo la umeme litakuwa limekwisha.



Serikali pia ilichukua maamuzi makubwa ya kubadilisha uongozi mzima wa mgodi na kuweka viongozi wapya ambao ni wawajibikaji, wazalendo na wenye uchu wa maendeleo ya kampuni na taifa kwa ujumla. Rais Dkt. John Pombe Magufuli amehakikisha wafanyakazi wote ambao ni viongozi katika makampuni ya serikali wanafanyakazi kazi kwa kufuata kasi yake na kuwa wazalendo kwa kuongoza kwa maslahi ya kampuni na serikali kiujumla na sio maslahi yao binafsi. Hapo nyuma kidogo mgodini haukufanya vizuri

hadi kufikia kiasi cha kutaka kufungwa kutokana na kuwepo kwa viongozi wasiokuwa wawajibikaji. Mgodini ulizalisha madeni mengi na kujiendesha bila faida na hivyo kupelekea hasara kubwa kwa serikali. Uamuzi wa Serikali ya Awami ya Tano umezaa viongozi wawajibikaji katika kampuni ya STAMIGOLD na kupelekea mgodini kufanya vizuri kila siku kwa kuzalisha dhahabu yenye kiwango bora na hivyo kuimarisha uchumi wa nchi ya Tanzania.

Mbali na hayo mgodi imechangia kutoa nafasi za ajira kwa raia wa kitanzania. STAMIGOLD inaendelea kuwa kioo kwa kutoa ajira kwa watanzania kwa asilimia 100. Kwa kipindi chote kumekuwa na watumishi 222 wenye fani mbalimbali. Mgodi unaendelea kutoa huduma muhimu kwa wafanyakazi wake kama malazi, chakula, bima za afya kwa ajili ya matibabu n.k.

Mgodi umetoa motisha kwa watumishi wake kwa kutoa *bonus* kila wanapofikia malengo ya uzalishaji. Pamoja na hayo mgodi umejipanga kuongeza mishahara kwa watumishi wote ikiwa ni njia ya kuongeza morali ya kufanya kazi. Mbali na hayo mgodi pia umefanikisha kuingia kwenye makubaliano na benki ya CRDB ambapo sasa watumishi wanaweza kupata mikopo (Salaried Loans).

Vilevile mgodi umekuwa darasa kwa mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi kutoka taasisi za elimu na vyuo mbalimbali vya elimu nchini, ambapo umeweza kuwahudumia wanafuzi 21 katika kipindi cha Januari mpaka Juni 2020.



STAMIGOLD imechochea ukuaji wa soko la ndani la dhahabu kwa kuwa mshiriki mkubwa kwenye masoko ya dhahabu yaliyoanzishwa chini. Uzalishaji unaofanyika mgodi hupelekwa moja kwa moja kwenye soko la ndani na sio kusafirishwa nje ya nchi kama ilivyokuwa hapo awali.